

# Uzio mnada wa kimataifa wa Pugu kukarabatiwa

Na REHEMA MAIGALA

**K**ATIBU Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, anayeshughulikia mifugo, Profesa Elisante Gabriel, amesema katika mwaka wa fedha 2020/2021, wanatarajia kufanya ukarabati wa uzio wa mnada wa kimataifa wa Pugu.

Amesema tayari wameshawaagiza wataalamu kufika katika eneo hilo kwa lengo la kuangalia miundombinu.

Profesa Gabriel, alisema hayo jana, alipozungumza na gazeti hili na kuongeza kuwa wanaupa kipaumbele ujenzi wa uzio wa mnada huo ili ulete tija kwa taifa.

Katibu Mkuu huyo, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuweka uzio katika mnada wa kimataifa wa Pugu, kwa kuwa ni moja ya kitega uchumi kwa taifa.

Alisema ujenzi wa uzio wa mnada

huo, utaleta tija na kukidhi mahitaji ya wafanyabiashara.

"Pamoja na mambo mengine aliyonituma Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, kuja kuangalia kwa umakini ni suala la uzio. Tutaona jinsi gani ya kuanza mwaka huu wa fedha kwa kuanza kazi hiyo, nimeshawaelekeza wataalamu waje kuangalia miundombinu ili wajue nini cha kufanya," alisema.

Akizungumzia ubovu wa barabara kutoka Gongo la Mboto hadi mnada wa Pugu, Profesa Gabriel, alisema hiyo ni changamoto nyingine.

Alisema tayari ameshafanya mazungumzo na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na kuahidi watalishughulikia.

Profesa Gabriel, alisema changamoto ya ukosefu wa maji, nayo anaichukua kwa ajili ya kuifanyia kazi kwa kutafuta njia itakayosalidia

uwepo wa maji ya uhakika, kwa ajili ya kunyweshea mifugo.

Alielekeza kuanza kutumika mara moja sehemu ya kupakia mifugo kwenye malori, ambayo ujenzi wake umekamilika licha ya uwepo kwa baadhi ya marekebisho.

Alisema ni vyema sehemu hiyo ikaanza kutumika kwa sababu

wafanyabiashara wamekuwa wakilalamikia kupata wakati mgumu wanapopakia na kushusha mifugo.

Awali, wafanyabiashara katika mnada huo waliiomba wizara hiyo lendelele kutatua changamoto zilizopo.

Baadhi ya wafanyabiashara waliiwasilisha kero zao kwa Katibu Mkuu, walisema wanakibiliwa na changamoto ya upatikanaji wa maji ya uhakika kwa ajili ya kunyweshea mifugo yao na uzio wa mnada.

## MIFUGO

# Pugu Mnadani walilia maji, barabara

**Dar es Salaam.** Wafanyabiashara katika Mnada wa Kimataifa wa Pugu jijini hapa wamelalamikia kukosekana huduma ya maji, hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Malalamiko hayo wamemweleza katibu mkuu wa Wizara ya Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel alipowatembelea kusikiliza kero walizonazo. Wameiomba Serikali kutatua changamoto hiyo pamoja na ubovu wa barabara ili mnada huo uwe na tija zaidi kwa maendeleo ya Taifa.

"Tatizo kubwa hapa ni maji kwa ajili ya mifugo. Viongozi kadhaa warmewahi kuja hapa, pamoja na kuchimba kisima na kuwekwa birika



Ia kunyweshea mifugo lakini hayawahi kutoka hata siku moja. Nashauri lirekebishwe lambo ambalo limekuwa likitumiwa siku nyingi tutakuwa na uhakika wa maji," amesema Said Waziri, mfanyabiashara mnadani hapo.

Akijibu kero hizo, Profesa Gabriel amesema uzio wa mnada utakarabatiwa kuanzia mwaka huu wa fedha 2020/21 na kukamilishwa 2021/22.

"Waziri amenituma kuja kuangalia kwa umakini sana, ni suala la uzio, tutaanza mara moja na nimeshawaelekeza wataalamu waje kuangalia nini cha kufanya," amesema Profesa Gabriel.

Kuhusu ukosefu wa maji, atalifanya kazi suala hilo kwa kutafuta njia itakayoweza kumaliza kero iliyopo.

**(Bakari Kiang'o)**